

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

Mji wa Serikali - Mtumba, Barabara ya Afya, S. L. P 573 - 40478 Dodoma.

Simu Na: 255(026)2963341/2963346, Nukushi: 255(026)2963348

Barua Pepe: ps@jamii.go.tz, Tovuti: www.jamii.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MARUFUKU YA KUWATUMIA WATOTO KATIKA SHEREHE NA BURUDANI
ZINAZOHAMASISHA VITENDO VYA MMOMONYOKO WA MAADILI UNAOHARIBU
MILA, DESTURI NA UTAMADUNI WA KITANZANIA

Ndugu Wananchi, katika siku za hivi karibuni kumeibuka mtindo katika baadhi ya maeneo ya hapa nchini, ambapo baadhi ya waandaji wa sherehe na burudani mbalimbali wamekuwa wakiwatumia watoto hasa wa kiume kufanya maonesho ya mienendo ya kike, jambo ambalo halikubaliki na linakinzana na misingi ya malezi na makuzi bora ya watoto, utu wao, mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania na kwa ujumla, ni kielelezo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Ndugu Wananchi, kitu cha kushangaza zaidi ni kuwa watu wanaohudhuria sherehe na burudani hizo, pasipo kujali madhara yake kwa watoto, huwaalika washereheshaji wanaochochea mihemko ya watoto hao kufanya vitendo hivyo, huku wengine wakiwarekodi watoto wanapofanya maonesho hayo yasiyofaa na kusambaza video hizo mitandaoni. Hali hiyo inaweza kuchangia tabia hizo kuonekana kuwa ni za kawaida na hatimaye kuzoeleka katika jamii.

Ndugu Wananchi, Serikali kupitia Wizara yenye dhamana ya malezi, makuzi na maendeleo ya watoto, haiwezi kuendelea kufumbia macho kuendelea kwa vitendo hivyo vya mmomonyoko wa maadili miongoni mwa makundi mbalimbali katika jamii, ambapo baadhi wameanza kurithisha mienendo hiyo kwa watoto hasa wa kiume, ambao kimsingi ndio nguvu kazi ya Taifa letu sasa na baadaye. Hali hiyo haikubaliki.

Ndugu Wananchi, kufuatia hali hiyo:

1. Nakemea vikali na kupiga marufuku tabia ya kuwatumia watoto hasa wa kiume kwenye matukio ya sherehe na burudani mbalimbali zinazohamasisha vitendo vya mmomonyoko wa maadili unaoharibu mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania. **HAZIFAI.**
2. Waandaji wa sherehe au burudani za aina hiyo wanaelekezwa kujisalimisha wenyewe katika Kituo cha Polisi kilicho karibu nao kabla ya tarehe 19 Agosti, 2026. Vinginevyo, nitawasilisha maombi rasmi kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ili Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wananchi wenye mapenzi mema lifanye msako wa kuwabaini wahusika na kuwasogeza mbele ya sheria.
3. Maafisa Utamaduni na Watendaji wa Serikali za Mitaa na Vijiji kote nchini, mnaombwa kuongeza umakini wakati wa uchambuzi wa maombi ya vibali vya sherehe na burudani ili kubaini viashiria vya mienendo hiyo na kutupilia mbali maombi yenye mashaka, ikiwemo yale yanayohusisha wanaume

wanaojigeuza na kufanya mienendo ya kike, kuwatumia watoto katika maonesho yasiyofaa, pamoja na sherehe zenye michezo ya kuvua nguo hadharani. Vitendo hivyo siyo tu vinakinzana na mila, desturi na utamaduni wa Kitanzania, bali pia ni kinyume na sheria na kanuni za nchi yetu. Pale ambapo ukiukwaji utathibitika, hatua stahiki zichukuliwe kwa mujibu wa sheria.

4. Aidha, natoa wito kwa wananchi wenye mapenzi mema kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa pale wanapobaini uwepo wa sherehe au burudani za aina hii. Ni vyema taarifa zitolewe wakati shughuli hizo zinaendelea na iwapo ikishindikana, basi taarifa zenye maelezo yaliyokamilika zinaweza kutolewa hata baada ya shughuli hizo kufanyika.

Ndugu Wananchi, wajibu wa kulinda maadili ya jamii na kunusuru vizazi siyo wa Serikali pekee, bali unaanzia kwa kila mwananchi kutimiza wajibu wake katika malezi na makuzi ya watoto, kuwa mfano mwema, kubaini mapema vitendo vinavyochochea vitendo vya mmomonyoko wa maadili na kuvikemea, sambamba na kutoa taarifa kwenye vyombo rasmi kwa mujibu wa sheria.

Ndugu Wananchi, nitoe rai kwenu kuwa mfano wa kuigwa kwa kukataa kutoa ushirikiano wa michango, hamasa, kuwa wafuasi wa vitendo hivyo mitandaoni au kushiriki katika sherehe na burudani za aina hiyo, kwa kuwa hatua hizo zinaweza kuvipa nguvu na kuhalalisha vitendo vinavyochochea mmomonyoko wa maadili katika jamii na Taifa kwa ujumla.

Ndugu Wananchi, asanteni sana kwa ushirikiano.



Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE
NA MAKUNDI MAALUM**

16 Agosti, 2026